

**HOTUBA YA MGENI RASMI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU
YA MTOTO WA AFRIKA KIJJI CHA MBUYUNI KATA YA MBUYUNI
TAREHE 16/06/2017**

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kijiji
Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM (W),
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri (W),
Mkurugenzi Mtendaji(W)
Waheshimiwa Madiwani,
Katibu Tawala (W),
Wakuu wa Idara
Afisa Tarafa.
Mtendaji wa Kata.
Wananchi wote mabibi na mabwana.
Asalaam aleikhum,
Bwana Yesu Asifiwe,
Habari za asubuhi.

Kwanza namshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa wote tukiwa na furaha kwa ajili ya watoto wetu. Naamini na kumuomba aendelee kutulinda na kuifanya siku yetu ikaishe salama.

Kama mlivyosikia toka kwa Mkurugenzi kuwa leo ni Siku ya Mtoto wa Afrika. Siku ambayo ilianzishwa rasmi kama kumbukumbu ya watoto waliofariki huko Afrika Kusini miaka 41 iliyopita. Kwa hiyo ndugu zangu wana Masasi na watanzania kwa ujumla tuone siku hii ni muhimu kwetu wazazi lakini muhimu kwa watoto wetu pia maana siku hii inatupa fursa muhimu ya kujadili maendeleo na changamoto zinazowakabili watoto kwenye maeneo mbalimbali nchini mwetu hususani wilayani kwetu.

Hivyo katika wilaya yetu ya Masasi kilele cha maadhimisho haya yanafanyika hapa kwenye kata ya Mbuyuni.

Kauli mbiu ya maadhimisho haya kwa mwaka huu ni **“MAENDELEO ENDELEVU 2030 IMARISHA ULINZI NA FURSA SAWA KWA WATOTO”**

Ndugu zanguni;

kauli mbiu hii inatutaka sisi kama jamii tuimarisha ulinzi kwa watoto wote, pale inapoonekana kuna dalili za kulegalega au kusuasua kwa namna moja au nyingine katika usalama wa mtoto basi hatua za haraka za kimalezi au kisheria zifuatwe. Pamoja na ulinzi pia yatupasa tupinge mambo yote yanayohatarisha ustawi na usalama wa watoto wote. Kauli mbiu hii inazidi kutukumbusha sisi kama wazazi/walezi na jamii kwa ujumla kuwa tunawajibu wa kuwafanya watoto wetu wawe na furaha wakati wote kwa kuwapenda na kuwajali kwa kuwapa mahitaji yote ya lazima ikiwemo chakula, mavazi, malazi na elimu. Tukiyafanya haya yote tutakuwa tunaishi ndani ya kauli mbiu yetu **“MAENDELEO ENDELEVU 2030 IMARISHA ULINZI NA FURSA SAWA KWA WATOTO”**

Ndugu wananchi

Katika hotuba yangu nitazungumzia kwa undani masuala ambayo jamii inapaswa kuyafanya ili kuongeza ulinzi na furaha sawa kwa watoto wetu.

Nikianza na suala la unyanyasaji kwa watoto wetu;

Ndugu zangu unyanyasaji unaweza kuwa wa kimwili mfano kuwapiga, kuwajeruhi, kuwachoma moto au mambo yote yanayopelekea kuwaumiza na kuwadhuru watoto wetu. Lakini pia unyanyasaji unaweza kuwa wa kijinsia kama kuwanyanyasa kingono, kuwabaka au kuwaingilia kimwili watoto wa kike au wa kiume na mwisho unyanyasaji unaweza kuwa wa kihisia mfano kutukana mbele za watoto au kupigana, kuwatisha, kuwapuuza, kuwatenga au kuwafanya vichekesho.

Vitendo hivi vyote tukivichekea na kuvichukulia kama ni vya kawaida kwa kiasi kikubwa vinapelekea kuzorotesha ulinzi na furaha kwa watoto wetu na madhara yake yanaweka madoa makubwa kwenye mioyo ya watoto wetu na ambayo yatakuwa ni vigumu kufutika na hatimae taifa linakuwa na wananchi waliobeba visasi na hawatakuwa katika jamii inayopanga mipango yao ya maendeleo vizuri.

Hivyo nitoe rai kwa wazazi,walezi na jamii nzima inayowazunguka watoto tusimamie sana makuzi ya watoto na tuwe mstari wa mbele kupinga na kukemea vitendo vyote viovu bila hofu wala woga wowote.

Pili ni suala la elimu kwa watoto wetu

Ndugu wananchi,

Hakuna kitu chenye thamani na urithi bora kwa watoto kama elimu, tujitahidi kufanya suala la elimu liwe kipaumbele cha kwanza kwenye kila familia. Tuhakikishe tunawapeleka watoto wetu kwenye programu za elimu ya awali (daycare center), elimu ya awali (pre primary school), kuwapatia elimu ya msingi na sekondari ambayo kwa sasa serikali inatoa elimu hii kuanzia awali hadi kidato cha nne (4) bure. Lakini pia ni muhimu watoto wanaomaliza darasa la saba kuwapeleka kwenye shule za ufundi stadi kama hawatachaguliwa kuendelea na shule za sekondari.

Mwisho fursa ya kupata elimu itolewe sawa kwa watoto wote bila ubaguzi kwani kuna baadhi ya wazazi kwa makusudi huamua kutowapeleka shule baadhi ya watoto hasa wa kike au walemavu.

Tatu kulinda afya za watoto wetu

Ndugu wazazi/walezi na jamii kwa ujumla tuhakikishe mazingira wanayoishi watoto wetu yanakuwa safi na salama, lakini ni vema pia kuzingatia usafi wao wenyewe; mavazi yao na hivyo kuwajengea afya bora.

Pia yatupasa tuwe wepesi kuwapeleka watoto wetu hospitali pindi tu wanapougua lakini tuisite kuwapeleka watoto wetu kupata chanjo za magonjwa mbalimbali kama inavyoelekezwa na wataalam katika kampeni mbalimbali kwa magonjwa kama kifua kikuu, polio, kifaduro, ndonda koo, homa ya ini, tetenasi n.k, kwani chanjo hizi husaidia kuzuia watoto wasiambukizwe au kuathiriwa na magonjwa hayo. Hinyo watoto hupata ulinzi wa afya zao na kudumisha furaha ya familia.

Suala la nne ni utekelezaji wa watoto

Ndugu zangu wazazi/walezi na jamii kwa ujumla; kumekua na tabia endelevu ambayo imejengeka kwa baadhi ya wazazi kuwatelekeza watoto wao kwa kukwepa kutoa mahitaji ya msingi kwa watoto kama vile chakula, mavazi, malazi na usimamizi ambao hupelekea kuwa na watoto wa mtaani lakini pia kupelekea watoto kuwa ombamba na mwishowe maisha na maendeleo ya watoto wetu kuwa hatarini. Nawasihi sana wazazi/walezi wenzangu tubadilike na tuache tabia za kutekeleza watoto wetu.

Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla tujitahidi sana kuwapatia malezi bora watoto wetu kwa kuwapa mahitaji ya kila siku hasa kuwapatia chakula bora chenye virutubisho muhimu ambavyo vitawapa watoto kinga ya mwili lakini ni vyema chakula kikazingatia makundi maalumu ya chakula kwa watoto ambayo ni pamoja na vyakula vyenye protini kwa wingi, wanga, mafuta, na kabohadrate ili kuwawezesha watoto wetu wakue vizuri.

Suala la Tano ajira kwa watoto

Ndugu wananchi,

Ninao uhakika kuwa mnafahamu kabisa suala la ajira kwa watoto. Wapo watu huwaajiri watoto majumbani, viwandani na mashambani shughuli za machimboni n.k. Nawaasa tuepuke kuwaajiri na kuwafanyisha kazi ngumu watoto wetu lakini pia tuungane kwa pamoja kupinga ajira kwa watoto au watoto kufanyishwa kazi zozote zinazo hatarisha maisha yao Ni vema watoto wetu wakasaidia kazi ndogondogo tu za nyumbani na si vinginevyo ili wapate muda wa kucheza na kujisomea.

Lakini ningependa kutoa ujumbe kwa wazazi/ walezi na jamii nzima kuwa baadhi ya mambo tukiwafanyia watoto wetu yatadumisha furaha na kujihisi wanajaliwa, Ndugu zangu watoto wanastahili ,upendo na kupendwa, kutambiliwa, kuthaminiwa.

Mwisho, ndugu zangu wananchi kuimarisha ulinzi na furaha kwa watoto ni jukumu la kila mmoja wetu na hakuna anayeruhusiwa kumdhuru au kumnyanyasa mtoto. Atakayeona mtoto/watoto wanaonewa au kutendewa vibaya asisite kutoa taarifa kuhusu vitendo hivyo kwenye ofisi za serikali za vijiji na kata, ustawi wa jamii, polisi, dawati la jinsia na timu ya ulizi na usalama wa mtoto

***“MAENDELEO ENDELEVU 2030 IMARISHA ULINZI NA FURSA SAWA
KWA WATOTO WOTE”***

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA